**LEARNING BY EAR**

**"Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii"**

**Episode 6: "Matokeo"**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION**

- **Beri (f, 45)**
- **Inspekta Tino (m, 40)**

**SCENE TWO: MORNING AT CHUNGA SANA BUS STOP**

- **Jabali (m, 18)**
- **Chambo (m, 30)**

**SCENE THREE: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S**

- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Bamju (m, 40)**

## SCENE FOUR: CHAMBO AND JABALI AT THE REHAB CENTRE

- **Jabali (m, 18)**
- **Chambo (m, 30)**
- **Jane (f, 35)**

## SCENE FIVE: AT THE POLICE STATION

- **Beri (f, 45)**

**MSIMULIZI (m/f)**

**INTRO:**

Nakusalimu nikikukaribisha tena katika Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki kikiwa ni kipindi cha sita katika tamthilia inayoendelea kuhusu mihadarati na vileo kwa jina **"Poromoko la jamii".** Kipindi kilichopita tuliona wanawake wa Chunga Sana wakiandamana kulalamika juu ya waume zao, ambao pombe haramu ilikwisha wafanya geu geu. Inspekta Tino alipigwa na mshangao mkuu, pale mkubwa wake Beri alipojiunga na waandamaji hao. Baadaye, Puyanga alitiwa mbaroni na mke wake Beri kwa mashtaka ya kujihusisha na biashara ya mihadarati. Jabali akajitolea kumsaidia Chambo katika kazi yake ya Youth watch inayoelimisha vijana kuepuka mihadarati na pia kuwashauri waathirika wa madawa haramu na vileo. Kwengineko, rafiki wa Jabali, Zula na Okosho wameanza kuishi maisha ya hali ya juu. Lakini hii itaendelea kwa muda gani? Tutambue yote katika kipindi cha leo, kiitwacho **"Matokeo".** Tunaanza na simu ya dharura kutoka kwa Bamju ambaye hakuwa na habari Puyanga kakamatwa na polisi.

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION**

1. **BERI:** **(tough and firm voice)** Inspekta Tino! Una hakika Bidhaa zote za Puyanga uko nazo?

2. **INSP. TINO:** Ndio, mkubwa. Inaonekana mumewako ni tajiri sana lakini njia za kupata hiyo mali ndiyo hazijulikani.

3. **BERI:** Tafadhali, Inspekta, wacha kumuita mumewangu. Kwa sasa yeye ni mshukiwa.

4. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

5. **BERI:** **(hurriedly)** Hiyo ni simu yake! Ninajuwa mlio wake. Hebu angalia nani anapiga, lakini usijibu.

6. **INSP. TINO:** Bamju anapiga! Nilikwambiaje – nilijuwa anahusika na madawa ya kulevya. Nimejaribu sana kumkamata. Tufanyeje?

7. **BERI:** Kata simu. Ni muhimu tufikirie kidogo jinsi ya kutatua kesi hii.

8. **INSP. TINO:** Pole sana kwa haya, Beri. Wewe ni kielelezo kizuri cha kikosi cha polisi. Nakuvulia kofia afande.

9. **BERI:** Ah, wacha kunihurumia! Kazi iko uko nje, kuna haja ya kwenda na kuzuia watu wasiuze madawa ya kulevya ili kuharibu maisha ya wananchi.

10. **SFX: SAME MOBILE PHONE RINGING AGAIN**

11. **INSP. TINO:** Bamju tena. Inaonekana hana subira mwenzetu.

12. **MSIMULIZI:** Kweli, sio subira tu, bali wasiwasi pia uliomwingia Bamju. Alihitaji madawa ya kulevya zaidi kwani biashara inanawiri – akashindwa kwanini hampati Puyanga? Kwengineko, asubui hiyo, katika kituo cha basi cha Chunga Sana, Jabali alimpata Chambo akiwa anamsubiri.

## SCENE TWO: MORNING AT CHUNGA SANA BUS STOP

**13. SFX: BUS STOP AMBIENCE, MORNING**

**14. CHAMBO:** Yani siku yako ya kwanza, na umechelewa kazini

**15. JABALI:** Kumradhi. Habari za asubui.

**16. CHAMBO:** Za kwangu njema. Una hakika uko tayari? Nakuahidi haitakuwa kazi rahisi.

**17. JABALI:** Niko tayari. Leo nitafanya nini?

**18. CHAMBO:** Nina kipindi cha ushauri leo katika kituo cha kubadili tabia na waathiriwa wa mihadarati, kisha mkutano wa viongozi wa kituo hicho, alafu baadaye mihangaiko yangu ya kawaida.

**19. JABALI:** **(takes a deep breath)** Sawa. Twende kazi!

**20. MSIMULIZI:** Ingawa juhudi nyingi zimefanywa, walakin Afrika ingali nyuma kwa masuala ya waathiriwa wa mihadarati na jinsi ya kuwasaidia . bado tunahitaji wataalamu wa ushauri, vifaa, matibabu na huduma ili kumudu idadi ya waathiriwa hawa. Hata Chambo ana mafunzo kidogo. Lakini kwanza, tuone jinsi Okosho na Zula watakavyozichukuwa habari mbaya.

**SCENE THREE: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S**

**21. SFX: HEAVY BANGING ON A TABLE (studio)**

**22. OKOSHO:** **(furious)** Unamaanisha nini, humpati muuzaji? Twahitaji mali, tena sasa hivi!

**23. BAMJU:** **( calm but threatening)** Kijana, chunga mdomo wako! Nilikwambia, sijui ni kwanini hachukui simu yangu. Nimejaribu mara mia moja na moja.

**24. ZULA:** **(speaking sluggishly – he is "high")** Aah… labda …labda…Labda amekufa. Unajuwa, kama… kama ... katika sinema, mameni.

**25. OKOSHO:** **(suddenly begging)** Tafadhali. Twahitaji bidhaa, Bamju. Tafadhali tusaidie. Hauoni twateseka? Hatuwezi kufanya chochote bila dozi yetu ya kila siku. Tafadhali tusaidie, tafadhali. **(almost in tears)**

**26. (ZULA is heard snoring)**

**27. BAMJU:** **(angrily)** Nje! Tokeni nje, nyote wawili! Bure sana, makabeji ya bei duni. Kazi kwisha. Nyinyi tayari mumekuwa waathiriwa. Niliwaonya heroini sio ubani wa kutafuna. Nje!

**28. OKOSHO:** Tafadhali… Tafadhali, Bamju!

**29. ZULA:** **(as if in a dream, still sluggish)** Okosho, Nini... kuna nini tena kilichotokea mameni?

**30. BAMJU:** Hakuna kilichotokea! Au kitakachotokea. Na sitaki kuwaona tena hapa kwangu. Mumenielewa?

**31. SFX: DOOR OPENED, THEN CLOSED AND LOCKED; NOISE OF TOWN IN BACKGROUND**

**32. OKOSHO:** **(thinking aloud)** Hapana, haiwezakani… nakumbuka... Bamju akisema kuna wauzaji unga wengine hapa Chunga Sana. Ni lazima tuwatafute watuuzie dozi yetu. Lakini pesa je? Tutapataje kama hatuna kazi? Hmm… nishajua. twenzetu, mameni Zula, tukachape kazi.

**33. MSIMULIZI:** Moja ya matokeo ya utumizi wa mihadarati na vileo, ni kwamba humgeuza mtu kuwa mhalifu. Tayari tunaona dalili hizi kwa Okosho na Zula ambao washaathiriwa na madawa. Watafanya nini ili kujipatia “dose” yao? Zidi kusikiliza. Si mbali sana na hapo, Jabali na Chambo walifika kwenye kituo cha kurekebisha waathiriwa, yaani “rehab centre” . Jabali alistaajabu kuona mtu wa kwanza aliyekuwa mwanamke kwa jina, Jane. Jane alikuwa na miaka thelathini hivi, na Jabali hakuelewa kivipi mrembo kama huyu kuishia mahala kama hapa.

**SCENE FOUR: CHAMBO AND JABALI AT THE REHAB CENTRE**

**34. SFX: 3 WOODEN CHAIRS BEING PULLED ACROSS THE FLOOR.**

**35. CHAMBO:** Habari, Jane. Nafurahi kukuona tena hii asubui.

**36. JANE:** Mzuri sana, Chambo. Ni nani huyu kijana mzuri? Ni kakako?

**37. CHAMBO:** Hapana. Ni mfanyakazi mwenzangu. Unaonaje kama akijiunga nasi?

**38. JANE:** Hamna tatizo. Angalau tupumue kwa kuona sura mpya.

**39. CHAMBO:** Vyema basi! Sawa, endelea basi, mweleze wewe ni nani. Kwa maana naona tayari damu zenu zimepatana.

**40. JABALI:** **(clears throat)** Kwa majina naitwa... ni… Jabali. Nashukuru kukujua!

**41. JANE:** Ni vyema kukujua, Jabali.

**42. CHAMBO:** Sawa. Sasa, tuanze basi? Jane, mbona usimueleze basi kwanini uko hapa.

**43. JANE:** Niko hapa kwa sababu nahitaji msaada. Nimeathiriwa na nikotini. Nikotini inapatikana katika bidhaa zote za tumbaku, nilianza kuvuta sigara tangu nikiwa shule ya upili. Nilipohitimu nilikuwa navuta paketi nzima kwa siku, baada ya hapo ndipo nikawa siwezi tena bila sigara. Majuzi nilianza kupata madhara katika afya yangu, na nilipochunguzwa na daktari, akanishauri niache sigara. Sio rahisi, lakini kwa ushauri wa Chambo naona maendeleo.

**44. CHAMBO:** Sasa unajisikiaje ?

**45. JANE:** Kichwa bado kinaniuma. Tamaa inapunguwa, lakini mwili bado unataka sigara.

**46. CHAMBO:** Jane, unaendelea vyema. Kumbuka, hamu ikikujia, ndio unafanyaje…

**47. JANE:** …najikumbusha tena na tena, kwanini nahitaji kuacha.

**48. CHAMBO:** Na unakumbuka sababu hizo, Jane? Kweli?

**49. JANE:** **(worried)** Naweza kujikumbusha kwa kusoma karatasi pale nilipoziandika?

**50. CHAMBO:** Bila shaka!

**51. SFX: PAPER TAKEN OUT OF A POCKET (studio)**

**52. JANE:** **(calmer, reading from paper)** Sababu ya kwanza: nawacha sigara kwa sababu zinahatarisha afya yangu na sitaki kufa kwa ajili ya nikotini. Pili, Naepuka sigara kwa sababu hazinidhuru mimi pekee, bali wote walio karibu yangu. Tatu,nawacha uvutaji kwa sababu ni ghali na siwezi matumizi haya. Nne…

**53. MSIMULIZI:** Jane akiendelea kunukuu sababu zake za kuacha uvutaji sigara. Jabali alitulia tuli, akimtazama, akamsikiliza, na kupendezwa mno na motisha alokuwa nayo Jane. Bamju, upande mwengine, alifikia pomoni.. kwa hivyo alifanya lile wengi wetu siku hizi hufanya wakati simu unayopiga haishikwi.

**SCENE FIVE: AT THE POLICE STATION**

**54. SFX: SMS RINGTONE AS WHEN A TEXT MESSAGE ARRIVES**

**55. BERI:** **(excited)** Shabash! Subira huvuta heri. Sasa, Bw. Bamju, umetuma ujumbe gani kwa mume wangu?

**56. SFX: BEEP TONE AS WHEN ONE OPENS A TEXT MESSAGE**

57. **BERI:** **(reads out) “**Bosi, kunaendelea nini? Najaaribu kukupigia sikupati. Mzigo wa leo sijaupata. Wafanyikazi wawili tayari nimewaachisha kazi. Au nikauchukuwe mzigo mwenyewe? Nasubiri unitume. Bamju”. **(thinking aloud)** Hmm…ndiyo sababu Puyanga anajiona ni mkurugenzi hata nyumbani. Hata hivyo – nifanyeje sasa? Hmm…

58. **SFX: BEEPS AS WHEN ONE TYPES A TEXT MESSAGE.**

59. **BERI:** **(talking as she types) “**Pole. Nimeshikika. Ndio,nenda kachukuwe mzigo mwenyewe. Unakujuwa kweli huko mzigo uliko? Puyanga” **(Pause)** Tuma ujumbe! Tafadhali…

60. **SFX: BEEP TONE AS WHEN MESSAGE IS SENT.**

61. **BERI:** Pole mumewangu, imenibidi nidanganye kidogo. Lakini la kuwa “umeshikika kidogo” si uongo. Sasa, wacha tuone kama Bamju ni mjinga kama ninavyodhania.

62. **MSIMULIZI:** Bamju alifurahia ujumbe kutoka kwa Puyanga, bila kujuwa ujumbe ule ulitoka kwa Beri, kule kituo cha polisi alikozuiwa Puyanga. Alimtumia ujumbe haraka Puyanga - na Beri karibu azirai.

63. **SFX: SMS TONE AS WHEN A TEXT MESSAGE ARRIVES**

**64. BERI:** **(impressed)** Lahaula! Haraka jinsi hiyo... Wacha tuone... **(reads text out again)** “Nashukuru kujuwa uko sawa. Ndio, nakumbuka ukinieleza mzigo uko kwa… **(sound of shocked disbelief)** Mjumbe wetu (*mbunge wa eneo letu*), Mheshimiwa Kizito. Kama kuna mabadiliko yeyote nieleze. Shukran Bosi – tuko pamoja”.

**OUTRO:**

Mshangao, hofu, kutoamini: Beri alihisi hisia hizi zote, na zaidi. Ngazi hii inaelekea wapi? Hakupoteza hata dakika moja, kwani alishafahamu kitu muhimu sana, lakini atachukua hatua gani? Atamgeukia nani, ikiwa waheshimiwa na wakuu wa serikali wanahusika katika hazma hii? Na je Okosho na Zula wanapanga nini ili kujipatia dozi yao? Bado Chambo na Jabali wako kule kwenye kituo cha kurekebisha waathiriwa madawa ya kulevya na kuna mengi yanayowangoja. Yote haya na mengine, ni katika kipindi kijacho. Kusikiliza tena hiki kipindi, au vingine vilivyorushwa hewani, tembelea tovuti zetu za www.dw.de/lbe Hadi wakati mwingine, kwaheri.